

**Ualishi wa Kuhudhuria Kongamano Jumuishi la Viongozi wa Makabila, Uongozi
Mbali Mbali na Wanachuoni wa Sudan Mashariki
(Imetafsiriwa)**

Mbali na fitna ya mizozo ya kikabila mashariki mwa Sudan, na kwa imani yetu kwamba Uislamu mtukufu, na kwa historia yote ya kibinadamu, kuwa ndio pekee utakaounganisha neno, na kuziunganisha safu na kuwayeyusha watu ndani ya chungu kimoja, bali hakika nidhamu za Uislamu ambazo Dola ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume itazitabikisha, ndizo njia pekee kufikia Maisha ya Kiislamu, salama na ya utulivu, ambamo matukufu yatahifadhiwa ndani yake, na nyoyo kuungana ndani yake, ikisadikisha maneno ya Mwenyezi Mungu (swt):

﴿وَأَلْفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مَا أَلْفَتْ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ أَلْفَ بَيْنَهُمْ إِنَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾

"Na akaziunga nyoyo zao. Na lau wewe ungesi toa vyote viliomo duniani usingeli weza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye waunganisha. Hakika Yeye ndiye Mtukufu Mwenye nguvu na Mwenye hikima." [Al-Anfal: 63]

Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan, inawaalika kuhudhuria kongamano jumuishi la viongozi wa Makabila, uongozi mbali mbali na wanachuoni wa Sudan Mashariki, chini ya kauli mbiu:

﴿وَأَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا﴾

"Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane." [Aali-Imran: 103]

Mahali: Mji wa Gadharif - Ukumbi (Wad Al-Barra) mbele ya jengo la manispaa ya Gadharif.

Wakati: Jumamosi 21/11/2020 kuanzia saa 9:30 Asubuhi hadi saa 3:30 Alasiri

Kuhudhuria kwenu ni tofali katika jengo la maisha ya Kiislamu

**Ibrahim Uthman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Sudan**